# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
## MAMLAKA YA KUDHIBITI NA KUPAMBANA NA DAWA ZA KULEVYA

Simu Nambari: 2152532/3
Fax Na: 2152820
*(Mawasiliano yote ya kiofisi yaandikwe
Kwa Kamishna wa Mamlaka)*

8 Barabara ya Kivukoni,
S.L.P. 80327,
**DAR ES SALAAM.**

**TAARIFA KWA UMMA**

**TAARIFA YA UKAMATAJI DAWA ZA KULEVYA MWEZI SEPTEMBA**

**Dar es Salaam, Septemba 23, 2019.**

Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya imefanikiwa kukamata dawa za kulevya aina ya Heroin zaidi ya Kilo moja na nusu katika Mikoa ya Dar es salaam na Mwanza pamoja na zaidi ya kilo 214 za vifurushi vya dawa za kulevya aina ya mirungi zilizokuwa zikisafirishwa kwa njia ya Posta kutoka Arusha kwenda nchini Uingereza.

Ukamataji huu wa usafirishaji wa vifurushi vya dawa za kulevya aina ya mirungi kwa njia ya posta ni muendelezo wa ukamataji uliofanywa na Mamlaka kwa kushirikiana na Shirika la Posta, Wizara ya Kilimo na Mifugo na Wizara ya Mali ya Asili na Utalii nchini ambapo zaidi kilo **300** za dawa za kulevya aina ya **Mirungi** iliyokuwa ikiingizwa nchini kutokea Ethiopia na kusafirishwa kwenda nchi za Ulaya hasa Uingereza kwa njia ya Posta, kwa kutumia majina bandia ya ***mlonge, moringa tea, dawa, majani ya mboga, tea leaves na moringa leaves***.

Pia, Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya kwa kushirikiana na Jeshi la Polisi inamshikilia aliyekuwa Afisa Usalama wa Shirika la Posta Tanzania **George Arsein Mwamgabe** kuhusiana na usafirshaji wa dawa za kulevya kwa njia ya Posta ambaye awali alitoweka kufuatia mahojiano yaliyokuwa yakiendelea dhidi yake. Pamoja na watuhumiwa sita (6) wanaohusishwa na dawa za kulevya aina ya Heroin uchunguzi wake umekamilika na watafikishwa Mahakamani.

Uchunguzi wa kimaabara kutoka kwa **Mkemia Mkuu wa Serikali** ulithibitisha, majani hayo yana kemikali aina ya **cathinone** ambayo inapatikana kwenye mmea wa mirungi (**Cath edulis)**. Taarifa za awali zilibaini kuwepo kwa usafirishwaji wa kiasi kikubwa cha dawa za kulevya aina ya mirungi kutoka nchini kwenda nchi za Ulaya kwa njia ya Posta, zikiwa zimepewa majina bandia, ambapo ilibainika dawa hizo ziliingizwa nchini kutoka nchini Ethiopia kama majani ya ***mlonge*** na kufungwa upya kisha kusafirishwa tena kwenda nchi za Uingereza, Canada, Ufaransa na nchi nyingine za Ulaya. Awali, vifurushi hivyo vilikuwa vikisafirishwa kupitia Posta ya Dar es salaam na sasa vimekamatwa vikisafirishwa kupitia Posta Jijini Arusha.

Mamlaka inatoa rai kwa wale wote wanaojihusishana na biashara ya dawa za kulevya waaache na watafute kazi halali za kufanya kwa sababu mkono wa Sheria utawafikia popote walipo na yeyeto mwenye taarifa itolewe kwa Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya.

**Imetolewa na,**

**Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano Serikalini**
**Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya.**